JARIDA MTANDAO LA ROBO YA KWANZA 2023/2024

# HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO

TOLEO NO 5

www.ubungomc.go.tz/Kitengo cha Mawasiliano Serikalini/Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo



## UBUNGO YETU, FAHARI YETU



# TAHARIRI

**Kongole kwa Vingozi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo kwa kufanikiwa kurejesha soko la Mabibo ambalo lilikabidhiwa kwa wananchi mnamo mwaka 2021 kutoka kwa aliyekuwa Rais wa awamu ya tano Hayati Mhe. Rais DKt. John Pombe Magufuli.**

**Sababu zilizopelekea soko hilo kurudi ni kutokana na malalamiko ya wafanyabiashara kuhusiana na Viongozi wa soko hilo kutoendesha soko hilo kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu ikiwemo kutosoma taarifa ya mapato na matumizi pamoja na kutofanya jitihada za kuboresha mazingira na miundombinu ya soko hilo huku wakiendelea kutoza wafanyabiashara hao ushuru mbalimbali sokoni hapo.**

**Manispaa ya Ubungo ilipokea rasmi tena soko hilo baada ya tamko la Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam Mheshimiwa Albert Chalamila kufika katika soko hilo tarehe 17/08/2023 kwa ajili ya kutatua migogoro iliyopo ikiwemo makusanyo ya tozo na ushuru ambazo wafanyabiashara walikuwa wanatozwa na Viongozi wa soko hilo huku maboresho ya soko yakiwa hayafanyiki**

**Tangu soko hilo lianze kusimamiwa na Manispaa ya Ubungo kiasi cha Shilingi Milioni 122,373,720 kimefanikiwa kukusanywa kwa kipindi cha miezi miwili agasti hadi oktoba toka kukabidhiwa soko hilo na ilitenga kiasi cha Millioni 600 kwa ajili ya maboresho ya soko hilo ikiwemo usafi wa mitaro, vyoo, usafi ndani ya masoko, ujenzi wa mabanda na kusimamia utawala bora unaozingatia sheria, kanuni na taratibu.**

**Alikadhalika, Manispaa ya Ubungo inapenda kuujulisha Umma kuwa mapato yanayopatikana katika soko hilo yataenda kuboresha miundombinu ya soko na pia kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kwa ajili ya maslahi ya wananchi wa Manispaa ya Ubungo na Taifa kwa ujumla.**

**Hakika Ubungo yetu ni fahari yetu.**

Tembelea Tovuti ya Ubungo Manispaa
www.ubungomc.go.tz



# HAMUWEZI KUNIPANDA KICHWANI, NINAO UWEZO WA KULIVUNJA SOKO - CHALAMILA

Na Mwandishi wetu

"Hamuwezi kunipanda kichwani"

Kauli hiyo ilitolewa na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mhe. Albert Chalamila 17 Agosti,2023 alipotembelea soko la mabibo na kuvunja uongozi wa Soko hilo na kukabidhi soko Manispaa ya Ubungo.

Soko hilo lilikuwa likimilikiwa na kikundi cha watu wachache nakupelekea kuwepo kwa changamoto mbalimbali ambazo Mkuu wa Wilaya Mhe.Hashim Komba alizibaini kama, miundombinu mibovu iliyo pelekea kuwepo kwa tope wakati wa mvua, chemba kuziba, mazingira machafu sokoni hapo, kutokuwepo kwa taarifa sahihi za mapato na matumizi, kutokuwepo kwa maboresho yoyote sokoni hapo huku kikundi cha watu wachache wakinufaika.

Katika mkutano huo, Mhe. Chalamila alianza kwa kuukemea vikari uongozi huo kwa mambo yaliyokuwa yanaendelea sokoni hapo ikiwemo kuwafukuza watumishi wa Serikali wanapotembelea soko hilo na hata kufikia hatua ya kutaka kuchoma moto gari la kubeba taka linalomilikiwa na Serikali.

"Hawawezi kutupanda kichwani, nimechukizwa na vitendo hivyo" alisisitiza Chalamila.

Aidha, Chalamila aliviagiza vyombo vya ulinzi na usalama kuhakikisha hakuna mtu yeyote atakaye kuja kusumbuliwa wakati

Inaendelea ukurasa wa 02.............




Inaendelea ........................................

Serikali ikifanya shughuli zake katika soko hilo kama ukusanyaji wa ushuru na uendeshaji wa soko hilo kiujumla.

Mhe.Chalamila alisema kuwa Soko litakuwa chini ya Manispaa na kuhakikisha hakuna mfanyabiashara atakaye sumbuliwa na mtu yeyote, taratibu zote zitaendelea kama kawaida, aliwaagiza wafanyabiashara sokoni hapo kulipa ushuru kwa Manispaa.

Baadhi ya wananchi na wafanyabiashara sokoni hapo wamepongeza hatua hiyo ya serikali ya kuchukuwa soko wakiamini soko hilo ninakwenda kuwa bora zaidi kama masoko mengine.

Aidha, Halmashauri imetenga kiasi cha shilingi Milioni 600 kwaajili ya kuboresha soko hilo na katika uboreshwaji huo hakuna mfanyabiashara yeyote atakaye ondolewa wakati uboreshaji unaendelea.




# MANISPAA YA UBUNGO YAANZA KAZI RASMI SOKO LA MABIBO

Na Mwandishi wetu

Kufuatia agizo la Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mhe. Albert Chalamila alilolitoa tarehe17 agosti,2023 la kuvunja uongozi wa soko la Mabibo na kulikabidhi kwa Manispaa ya Ubungo na kuagiza shughuli zote zilizokuwa zikifanywa na uongozi uliovunjwa Agosti 18, 2023 Manispaa imeanza kazi rasmi ya usimamizi wa soko hilo ikiwa ni pamoja na ukusanyaji wa mapato kama ilivyokuwa awali bila kufanya mabadiliko yoyote ya tozo hizo.

kutokana na mabadiliko hayo, wafanyabiashara wamepongeza hatua hiyo na kuonesha ushirikiano wa dhati kwa kutoa ushuru kwa Hiari. Kwa upande wa wafanyabiashara wa soko hilo wamepokea vizuri mabadiliko hayo na ni mategemeo yao kuwa Manispaa itafanya maboresho ya miundombinu kwenye soko hilo kwa wakati ili wawe na mazingira bora yakufanyia biashara

Esther Ngowi mfanyabiashara wa nyanya sokoni hapo anaeleza kuwa “Soko letu linahitaji maborecha mvua hatuuzi, humu ndani ni tope tu, kuna baadhi ya wateja wetu wanashindwa kufika humu ndani inapelekea mauzo kushuka. Labda kwa mabadiliko haya tutegeme chochote”.

Aidha, Esther alisema kuwa, Halmashauri kuanza kusimamia soko hili wafanyabiashara kuwajibika kutoa ushuru kwani tuna imani maboresho makubwa yatafanyika kwenye soko letu hivyo tutakuwa na mazingira Bora ya kufanyia biashara.

Kwa awamu ya kwanza, Manispaa imejipanga kuboresha soko hilo ambapo tayari kiasi cha shilingi milioni 600 zimeshatengwa kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya soko hilo ikiwemo ukarabati wa vyoo, ujenzi wa mitaro na ujenzi mabanda 12.

Halmashauri, iliwashukuru wafanyabiashara wa soko hilo kwa kuonesha ushirikiano kwa Manispaa kutekeleza majukumu ya kusimamia soko na kudumisha utulivu ndani ya soko.




# DC KOMBA AZINDUA KAMPENI YA "KATAA UCHAFU, SAFISHA, PENDEZESHA UBUNGO"

Na Mwandishi wetu

Rasmi kampeni ya "Kataa Uchafu, Safisha, Pendezesha Ubungo" KAU -SAPEU" ilizinduliwa Manispaa ya Ubungo kwa lengo la kuweka mazingira safi na salama.

Akizindua kampeni hiyo tarehe 26 agosti, 2023 iliyofanyika katika Kata ya Manzese Mkuu wa Wilaya ya Ubungo Mhe. Hashim Komba alisisitiza uondoaji wa taka katika maeneo yote kwa kuzingatia ulipaji wa pesa za taka ili magari yanayokusanya taka yaweze kuchukuwa taka kwa wakati na kila Mtaa kuzingatia usafi wa maeneo yao.

"Niwapongeze Kata ya Manzese kwa kuipokea vyema kampeni hii maeneo mengi tayari yamesafishwa". Alisema hayo Komba.

Aliendelea kwa kusema kuwa taka ngumu nyingi zinazalishwa kwa wingi na haziondolewi kwa wakati sambamba na utiririshaji wa maji taka.

Aliendelea kwa kusema kuwa, Katika kampeni hii kutakuwa na zawadi zitakazo tolewa kwa mwaka ambapo Pikipiki mbili zitatolewa, Pikipiki moja kwa Mtaa utakaofanya vizuri na ya pili mwenyekiti wa Mtaa.

Na kila baada ya miezi mitatu zawadi zitatolewa kwa mtaa utakaofanya vizuri wa kwanza shilingi 600,000/= wa pili 300,000/= na watatu 200,000/=

Na Kwa Mtaa ambao utafanya vibaya utapewa Bendera ambayo itasomeka "Balozi wa Uchafu Ubungo"

Nae, Mstahiki Meya Manispaa ya Ubungo Jaffery Nyaigesha alipongeza kuanzishwa kwa kampeni hiyo na kusisitiza ni lazima tupambane kukataa uchafu na sheria ya hakuna kutupa hovyo taka lazima ifuatwe.

"sheria hii lazima izingatiwe na ifatwe" amesisitiza Mstahiki.





# NAIBU WAZIRI WA MAJI ATEMBELEA MIRADI YA MAJI - UBUNGO

Na Mwandishi wetu

Naibu Waziri wa Maji Mhe. Eng. Maryprisca Mahundi  Agosti 20, 2023 alitembelea miradi ya Maji iliyopo Manispaa ya Ubungo, miradi iliyotembelewa ni pamoja na Tanki la Maji lililopo Mtaa wa Mshikamano Kata ya Mbezi lenye ujazo wa lita Milioni sita na kituo cha kusukuma maji kilichopo Mbezi inn.

Katika ziara hiyo Naibu waziri Mahundi alipokelewa na Mkuu wa Wilaya hiyo Mhe. Hashim Komba, akimpokea naibu waziri huyo Mhe. Komba amepongeza jitihada zinazofanywa na wizara katika kutatua kero za maji kwa wananchi. Moja ya maeneo hayo ni Tanki la maji la Mshikamano ambalo ni kwaajili ya maeneo kama Mbezi, Mshikamano, Msakuzi, Machimbo, Makabe, Luguruni na Magari saba.

pamoja na kujenga miundombinu ya maji safi "Spidi ya miradi ya maji iende sambamba na ujenzi wa mifumo ya majitaka". Alizungumzia eneo kama Sinza kiujumla na Hospitali ya Sinza, eneo hili linaitaji sana mifumo ya majitaka kwani eneo watu wengi na uzalishaji wa maji taka ni mkubwa.

Pia Mhe. Komba alisema kuwa jitihada zinaendelea kufanyika kutatua kero za maji, ali-

Inaendelea ukurasa wa 06................



Inaendelea ..........................................

ongeza kuwa kwa eneo hilo ni asilimia 40 tu ndiyo imekamirika na bado jitihada zinaendelea ili tatizo la maji limalizike kabisa.

Wananchi wa maeneo hayo pia wamepongeza juhudi zinazofanywa na Serikali ya awamu ya sita katika kutatua kero za maji katika maeneo yao. Wameongeza kuwa japo kuna changamoto lakini wanaimani mambo yatakuwa mazuri kwa juhudi wanazoziona zikiendelea.

Mzee Hondohondo mkazi wa maeneo hayo alishukuru kwa miradi hiyo mikubwa ya fedha nyingi lakini amesisitiza kuwa wananchi waungiwe maji kusiwe na danadana. Sambamba na hilo amegusia Shule ya Sekondari Makabe ipatiwe maji kwani ni Shule yenye wanafunzi wengi lakini kuna tatizo la maji.

Katika ziara hiyo Naibu Waziri amewaomba wananchi wa maeneo hayo kutunza miundombinu hiyo inayofanywa na Serikali ya awamu ya sita ili idumu kizazi hadi kizazi.

"Niwaombe sana wananchi, miundombinu hii itunzwe ili idumu kizazi hadi kizazi".





# MRADI WA UBORESHAJI USALAMA WA MILKI ZA ARDHI WATAMBULISHWA UBUNGO

Na Mwandishi wetu

Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi kupitia mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi (LTIP) inakusudia kupanga, kupima na kusajili hati za hakimiliki 28,000 mkoa wa Daressalaam

Hayo yameelezwa na Bi. Aisha Masanja mwezeshaji kutoka Wizara hiyo leo septemba 05, 2023 wakati akitambulisha mradi huo kwa timu ya menejimenti ya Manispaa hiyo.

Masanja amesema kuwa kwa Manispaa ya Ubungo mradi utaanza kutekelezwa katika Mitaa mitano ukiwemo Mtaa wa Saranga, Mbezi Louis, Stop over, Kimara B na Kibwehele ambapo jumla ya hati miliki 3,419 zitatolewa kwa wananchi wa Mitaa hiyo.

“Manispaa ya Ubungo ni miongoni mwa Halmashauri chache Nchini zilizobahatika kutekeleza mradi huu wenye tija kwa jamii kwani unalenga kuboresha usalama wa milki za ardhi kwa kupanga, kupima na kusajili hati za hakimilki pamoja na kupunguza gharama za upimaji” alisema Masanja.

Ili kuhakikisha wananchi wanapata hati kwa wakati, Masanja ameeleza kuwa kupitia mradi huu wananchi watafikiwa katika Mitaa yao na kuhakikisha mazoezi yote ya

Inaendelea ukurasa wa 08 ..................



Inaendelea ........................................

urasimishaji yaliyokuwa yameanza kupitia makampuni yanafika mwisho kwa watu kupata hati zao.

Akiongea wakati wa kufunga kikao hicho, Mkurugenzi wa Manispaa ya Ubungo Ndg. Elias Ntiruhungwa ameishukuru Serikali kwa mradi huo ambao unatoa fursa kwa wananchi kupimiwa na kumilikishwa maeneo yao kwa muda mfupi jambo ambalo ni kiu ya muda mrefu ya wananchi.

Aidha, Ntiruhungwa ameeleza kuwa upimaji na umilikishaji ardhi ni chanzo kikubwa cha mapato kwa Serikali hivyo ni mategemeo yake baada ya mradi huu kuisha maeneo yanayopitiwa na mradi yataanza kulipa kodi ya ardhi na hivyo kukuza uchumi wa Nchi.

Hata hivyo Ntiruhungwa ameahidi kuhamasisha wananchi kutumia fursa hii kwa kushiriki vyema katika utekelezaji wa mpango wa matumizi ya ardhi kupitia mradi wa uboreshaji usalama wa milki za ardhi.

Ntiruhungwa ameongeza kuwa "ikumbukwe zamani upatikanaji wa hati ulikuwa mgumu sana ,hivyo mradi huu utaleta matumaini kwani hati sasa zitapatikana ngazi ya mtaa ambapo wataalamu watakaa siku tano kwa kila mtaa kwa ajili ya kazi hiyo.



# MKURUGENZI NTIRUHUNGWA KWENYE UKAGUZI WA MIRADI, ATOA KIBALI KWA MAFAILI YA MUHIMU KUWAHISHWA

Na Mwandishi Wetu

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo Ndg. Elias Ntiruhungwa alifanya ziara ya ukaguzi wa kasi ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika maeneo mbalimbali.

Ntiruhungwa alikagua ujenzi wa awamu ya pili katika Shule ya Sekondari Dar es Salaam Girls, Shule ya Msingi Ubungo NHC na mradi wa uboreshaji wa awamu ya kwanza katika soko la Mabibo.

Akiongea na wahandisi wa mradi wa Dar es Salaam Girls ambapo kwa awamu ya pili kunajengwa mabweni manne, madarasa 10, nyumba za walimu za familia tano pamoja na chumba cha ICT, Ntiruhungwa alisisitiza suala zima la uwajibikaji, ushirikishwaji na wepesi kwenye kufanya maamuzi kwa maslahi mapana ya Manispaa.

"Nimetoa kibali kwa Mtumishi yoyote unapokua na jambo la muhimu, hakikisha umeshika faili mkononi unalileta kwangu ili nisaini na taratibu zingine ziendelee bila kuwa na kikwazo chochote" alisema Ntiruhungwa.

Aidha, katika mradi wa maboresho katika soko la Mabibo, Mkurugenzi Ntirihungwa ametoa kipindi cha wiki mbili kutoka leo mpaka inapofika Septemba 26, 2023 shedi hilo liwe limekamilika na kutumiwa na wafanyabiashara wa soko hilo, ambapo kauli hiyo imeungwa mkono na wafanyabiashara wa soko hilo ambao wamepongeza jitihada za Serikali kwenye kuboresha soko hilo.



# UBUNGO YAADHIMISHA SIKU YA USAFI WA MAZINGIRA DUNIANI

Na Mwandishi Wetu

Manispaa ya Ubungo tarehe 16 Septemba, 2023 imeadhimisha siku ya usafi duniani kwa kufanya usafi wa mazingira ya soko la Mabibo maarufu kama soko la ndizi

Maadhimisho hayo yameenda sambamba na kauli mbiu isemayo "Tuungane pamoja, kujifunza, kupanga na kuhimiza uimarishaji na udhibiti wa taka" na huo umefanywa na wadau mbalimbali ikiwemo Green awereness club, Suma JKT, wananchi ambao ni wajasiriamali wa soko hilo pamoja na viongozi mbalimbali.

Akiongea wakati wa usafi huo Mhe. Juma Jaffery Nyaigesha ameeleza kuwa Manispaa ya Ubungo imeendelea kuhakikisha maeneo yote yanakuwa safi na katika kuhakikisha hili linawezekana iliweka mikakati madhubuti ya utunzaji wa mazingira ikiwemo na Kampeni ya usafi wa mazingira ijulikanayo kama "kataa uchafu; safisha pendezesha Ubungo"

Mhe. Nyaigesha ametoa rai kwa wajasiriamali wa soko hilo sambamba na wananchi wote wa Manispaa hiyo kuhakikisha maeneo yao yanakuwa safi muda wote na kuendelea kutunza miundombinu ya soko hilo ambayo inaendelea kuboreshwa na Manispaa hiyo ili kuwezesha mazingira bora ya kufanya biashara.

Kwa upande wake Meneja wa soko hilo Samuel Lugala alieleza kuwa Manispaa ya Ubungo imetoa kiasi cha shilingi Milioni 600 kwa ajili ya maboresho ya soko na aliwataka wajasiriamali wa sokoni hapo kuendelea kushirikiana vyema na Manispaa ili kutunza miundombinu hiyo na mazingira yake huku elimu ya utunzaji wa mazingira ikiendelea kutolewa.

Nae Kelvin Marwa Mwenyekiti wa Klabu ya Green Awereness alisema klabu hiyo inajishughulisha na utoaji wa elimu ya utunzaji wa mazingira, matumizi ya nishati mbadala na upandaji wa miti kwenye Shule mbalimbali za msingi za sekondari pamoja na vyuoni.

Marwa aliendelea kueleza kuwa sambamba na kutembelea Shule na vyuo mbalimbali bado klabu hiyo imekuwa ikishirikiana na jamii kwa kufanya usafi kwenye maeneo mbalimbali, kupanda miti na kuielekeza jamii kutumia uchafu wa mabaki ya chakula kutengeneza mbolea pamoja na kutumia maboksi kutengenezea mkaa mbadala.





# DC KOMBA ATEMBELEA OFISI YA WAKALA WA BARABARA TANZANIA (TANROADS)

Na Mwandishi Wetu

Mkuu wa Wilaya ya Ubungo Mhe. Hashim Komba alifanya ziara katika ofisi ya wakala wa barabara Tanzania TANROADS kwaajili ya kujadili masuala mbalimbali ya miundombinu katika Wilaya ya Ubungo.

Miongoni mwa mambo makuu yaliyojadiliwa katika kikao hicho ni pamoja na kuweka mipango madhubuti ya matumizi ya maeneo ya hifadhi ya barabara, mpango wa upendezeshaji wa mji, ulinzi wa miundombinu pamoja na ushirikiano wa kutatua changamoto za miundombinu ya barabara.

Kwa upande wa TANROADS akiongea kati ka kikao hicho kaimu Meneja wa TANROADS Mkoa wa Dar es Salaam Injinia Elisony Mweladzi amemshukuru DC Komba kwa ziara hiyo na ameweka wazi kuwa ni Mkuu wa Wilaya wa kwanza kufanya ziara hiyo katika ofisi za TANROADS.

Ambapo ziara hiyo ililenga kutengeneza ushirikiano na utendaji kazi wa pamoja katika kuhakikisha kupatikana kwa matokeo chanya kwenye ujenzi bora wa miundombinu katika Wilaya ya Ubungo.



# UBUNGO YAJIPANGA KUONGEZA WANACHAMA BIMA YA CHF ILIYO-BORESHWA

Na Mwandishi wetu

Maafisa uandikishaji wa CHF iliyoboreshwa wa Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo wamejipanga kuendelea kutoa elimu kwa Wananchi ili kuongeza idadi ya wanufaika wa huduma za afya kutoka asilimia 7.6 ya sasa hadi kufikia asilimia 13 ifikapo Juni 2024.

Hayo yalibainishwa na Mratibu wa mfuko wa Bima iliyoboreshwa wa Manispaa ya Ubungo Bi. Reticia wakati wa kufungua kikao kazi kwa Maafisa uandikishaji wa Manispaa hiyo lengo likiwa ni kujadili na kupanga mkakati wa kuhamasisha utoaji elimu kwa jamii ili kuongeza idadi ya wanachama wa Bima hiyo na kuboresha huduma.

"Nimeona tukutane na tupange mikakati ya pamoja ya namna ya kuhamasisha jamii kujiunga na mfuko wa bima ya CHF iliyoboreshwa kwa kutoa elimu kwa wananchi katika maeneo mbalimbali yenye mikusanyiko ikiwemo Masokoni, Viwandani, Taasisi, Shule na Makampuni".

Aidha, Maafisa uandikishaji pia walisisitizwa kutumia mikutano na vikao mbalimbali ngazi ya Mitaa na Kata kutoa elimu kwa jamii, utaratibu wa kujiunga na faida za kutumia bima hiyo ya gharama nafuu sana kwa wananchi hasa wa kipato cha chini.

Pamoja na kutoa elimu hiyo kwenye mikusanyiko ya watu, Bi. Reticia amesema matumizi ya vyombo vya habari na matangazo ni moja ya njia watakayotumia kuelimisha wananchi wengi zaidi kujiunga na bima hiyo ambayo inamwezesha mwanachama -

Inaendelea ukurasa wa 13 ...........................




kupata matibabu kuanzia ngazi ya Zahanati hadi Hospitali ya Mkoa popote Nchini.

Aidha, alisema hadi kufikia Juni 2023 jumla ya wanachama 40384 wamejiunga na Bima ambapo kati ya hao 6516 wamejinga mwaka huu 2023.

Kuhusu matibabu , Bi. Reticia amesema hadi kufikia Juni 2023 jumla ya wanachama 12499 walipatiwa huduma za Afya kwenye vituo vya kutolea huduma ambapo jumla ya shilingi 185,330,000 zilikusanywa kutoka kwa wanachama na shilingi 65,374,991 zimerudishwa katika vituo vya kutolea hud-uma kwa ajili ya kuboresha utoaji huduma za afya vituoni.

Akiongea kwa niaba ya maafisa uandikishaji Bi. Sabina Balilo aliipongeza Manispaa kwa kuweka kikao hicho na kwamba kimeongeza chachu ya kujipanga vizuri kila mmoja kwenye eneo lake ikiwemo kushirikiana na viongozi kuanzia ngazi ya Shina, Wenyeviti wa mitaa na Kata.



# WAKUU WA IDARA NA VITENGO UBUNGO WAPEWA ELIMU YA MASUALA YA AFYA YA AKILI.

Na Mwandishi wetu

"Unywaji wa pombe kupita kiasi, msongo wa mawazo na uvutaji wa sigara ni moja kati visababishi vya matatizo ya afya ya akili kwa watu wengi"

Kauli hiyo ilitolewa tarehe 21/08/2023 na mtaalamu wa masuala ya afya ya akili Dkt. Isaac Lema alipokuwa akielezea masuala hayo kwa wakuu wa Idara na Vitengo Manispaa ya Ubungo lengo ikiwa ni kuwapa uelewa juu ya athari na namna ya kusaidia changamoto za afya akili sehemu za kazi.

Lema aliendelea kueleza kuwa pombe ina kiwango maalamu cha mtu kunywa na kikizidi kiwango hicho basi ni rahisi kumpelekea mtumiaji kupata tatizo la afya ya akili kutokana na uraibu wa unywaji wa pombe hizo.

Akifafanua Lema alieleza kwa wanywaji wa pombe kwa upande wa wanawake hawatakiwi kuzidisha chupa 2 za pombe kwa siku na zisizidi chupa 10 kwa wiki, na wanaume wasinywe pombe zaidi 3 kwa siku na zisizidi 15 kwa wiki huku wakizingatia namba ya kiwango cha kilevi cha pombe husika pamoja na mapumziko ya siku mbili kila wiki bila kunywa pombe huku wajawazito wakizuiliwa kunywa pombe hizo.

Aidha, Lema aliendelea kueleza kuwa madhara ya

Itaendelea Ukurasa wa 15...........................




Inaendelea ..........................................

matatizo ya afya ya akili yanaathari mbaya sana kwa Taifa na mara nyingi hupelekea mwenye tatizo hilo kupoteza maisha hivyo ni jukumu la kila mmoja kuelimisha jamii juu ya masuala ya afya ya akili.

Kwa upande wake Mganga Mkuu wa Manispaa hiyo Dkt. Tulitweni Mwinuka alipongeza Mtaalamu huyo kwa elimu hiyo muhimu aliyoitoa ambayokwa kiasi kikubwa itawezesha watumishi wa Manispaa hiyo kupata msaada juu ya masuala ya afya ya akili na ameeleza kuwa Idara ya afya kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itahakikisha wananchi wa Manispaa hiyo wanapata elimu hiyo yenye tija na manufaa kwa Taifa.

Sambamba na hilo Dkt. Mwinuka alitoa wito kwa wataalamu waliopata elimu hiyo kuwa mabalozi wakuhakikisha matatizo ya afya ya akili hayatokei na yanazuiliwa sehemu za kazi.



# WAMILIKI WA HOTEL WAIPA HEKO IDARA YA MAZINGIRA KWENYE MIPANGO YA UTATUZI WA CHANGAMOTO YA MAJI TAKA

Na Mwandishi wetu

Katika muendelezo wa mikakati ya kampeni ya "Kataa Uchafu, Safisha Pendezesha Ubungo" leo Agosti 23, 2023 idara ya mazingira na udhibiti wa taka Ngumu Manispaa ya Ubungo imefanya kikao na wadau wa mazingira kutoka kata ya Sinza, Ubungo na Manzese ili kujadili changamoto mbalimbali za taka ngumu zinazokabili kata hizo na njia bora ya kukabiliana nazo

Wadau walioshiriki kikao hicho ni pamoja na wamiliki wa hoteli na kumbi za starehe ambao hao ndo wadau wakuu wanaozalisha kwa wingi taka ngumu na kutiririsha maji taka kutoka katika maeneo yao ya biashara. Pamoja na wadau hao pia katika kikao hicho walialikwa viongozi wa DAWASA ambao ndio taasisi yenye wajibu wa kukabiliana na maji taka

Akiongea katika kikao hicho afisa tarafa ya Ubungo Ndg. Agnes Kyando ambaye alimuwakilisha mkuu wa wilaya ya Ubungo amesema kuwa wamiliki wa hoteli na kumbi za starehe ni wadau muhimu kuelekea kwenye kampeni ya "Kataa Uchafu, Safisha Pendezesha Ubungo" ambayo inatarajiwa kuzinduliwa Jumamosi ya Agosti 26, 2023 katika kata ya Manzese eneo la Bakhresa, hivyo wajitokeze kwa wingi ili kufanikisha kampeni hiyo.

Inaendelea ukurasa wa 17 ................



Inaendelea ....................................

Akiongea katika kikao hicho Mkuu wa idara ya Mazingira na udhibiti wa taka ngumu Manispaa ya Ubungo Lawi Benard ametumia kikao hicho kutengeneza uelewa wa pamoja wa changamoto za majitaka katika maeneo hayo ili kwa pamoja kutafuta suluhu ya kudumu

Kwa upande wa wamiliki, kwanza wameiongeza Manispaa ya Ubungo kwa kufanikisha kikao hicho ambacho wamekiri kuwa ni kikao chenye tija kubwa kwao kwa kuzingatia kuwa biashara zao zimekuwa zikikabiliwa na tatizo la maji taka kwa muda mrefu sasa

Aidha, wameuomba uongozi wa DAWASA kuhakikisha wanakuja na majawabu ya kudumu kwa changamoto hiyo ikiwemo kuwa na bomba kubwa la maji taka ili kukabiliana na kero ya majitaka kwa njia ya kisasa zaidi



**Pichani ni Mstahiki Meya wa Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo JAFFARY J. NYAIGESHA**



**Pichani ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo Ndg. ELIAS R. NTIRUHUNGWA**


PONGEZI
PONGEZI
PONGEZI
Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo inakupongeza Mhe. Mohamed Mchengerwa (MB) kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI
Manispaa ya Ubungo tunaahidi kukupa ushirikiano wa dhati katika utekelezaji wa majukumu yako kwa Maendeleo ya wananchi wa Manispaa ya Ubungo na Tanzania kwa Ujumla.
UBUNGO yetu
FAHARI YETU
www.ubungomc.go.tz


HALMASHAURI
YA MANISPAA
YA UBUNGO
ASANTE
MAMA
DAR ES SALAAM GIRLS
IPO TAYARI KWA MASOMO
YA KIDATO CHA TANO 2023
WANAFUNZI WOTE
MNAKARIBISHWA



# MRADI WA UBORESHAJI WA USALAMA WA MILIKI (LTIP) KUANZA RASMI UBUNGO

Na Mwandishi Wetu

Mradi wa urasimishaji kupitia benki ya Dunia rasmi unaenda kuanza katika Wilaya ya Ubungo na utafanyika katika mitaa yote 90.

Hayo yameelezwa na Komba alipofungua kikao kazi kilichojumuisha Wenyeviti wa Mitaa na Viongozi wa Kamati za Urasimishaji za Mitaa kilicholenga kuzungumzia maswala ya urasimishaji kwa Wilaya ya Ubungo.

Mhe. Komba aliendelea kwa kusema kuwa kwa mujibu wa World Bank urasimishaji utafanyika kwa kiasi cha shilingi laki moja na elfu thelathini "130,000" ambapo kila mwananchi atalipia fedha hiyo ambayo itakua ni kwa ajili ya utambuzi, upangaji na upimaji.

"Sasa Wenyeviti tembeeni vifua mbele urasimishaji unaenda kufanyika katika Wilaya ya Ubungo nendeni mkasimamie vyema zoezi hilo muhimu kwa wananchi" Alisema Mhe. Komba.

Komba aliendelea kwa kusema kuwa, natamani kuona Wilaya yetu ya Ubungo inaenda kufanya zoezi hili Kwa haraka na muda mchache.

Inaendelea Ukurasa wa 21 .............




Nataka Ubungo ikawe Wilaya ya mfano katika zoezi hili la urasimishaji na Mtaa utakaofanya maandalizi kwa haraka kwa kuhakikisha uundaji wa Kamati unafanyika kwa wakati basi nitakuja mwenyewe kwenye Mtaa huo kwaajili ya kufanya hamasa.

Nae, Mratibu wa zoezi la urasimishaji Wilaya ya Ubungo Ndg. John Ilomo alielezea Mradi wa uboreshaji wa usalama wa miliki (LTIP) kupitia Benki ya Dunia katika Halmashauri ya Ubungo lengo lake ni kukwamua zoezi la urasimishaji katika Mitaa kwa kukamilisha kazi na kutatua changamoto za kila Mtaa kulingana na hatua ya utekelezaji iliyofikiwa na Makampuni yaliyokuwa yakitekeleza miradi hii.

Aliendelea kusema kuwa, Ardhi clinic itafanyika katika ngazi ya mitaa ili kusogeza huduma za umilikishaji kwa wananchi ambapo mitaa mingi itafikiwa ikiwa ni pamoja na kufanya uhakiki wa taarifa zilizokusanywa wakati wa zoezi la urasimishaji.

Mradi huu pia umelenga kutoa hati kidigitali hivyo utahusisha pia zoezi la kubadilisha data kutoka katika mfumo wa zamani na kuzipeleka katika mfumo wa kidigitali utaanza rasmi kuanzia tarehe 17/9/2023.



## UBUNGO, KISARAWE WAKUTANA KING'AZI KUTATUA MGOGORO

Na Mwandishi wetu

Kufuatia mgogoro wa mpaka katika Mtaa wa King'azi A Kata ya Kwembe, Wakuu wa Wilaya za Ubungo na Kisarawe wameunda timu maalumu inayojumuisha wataalamu na wananchi wa pande zote mbili kwa ajili ya kupata uelewa wa pamoja kuhusu mipaka ya eneo hilo ambalo limekuwa na migogoro mingi ya ardhi kwa kisingizio cha mipaka ya eneo hilo.

Uundaji wa timu hiyo ni moja ya maazimio yaliyotolewa na wakuu hao wa wilaya septemba 9, 2023 kwenye mkutano wa wananchi wa mtaa huo ukilenga kusikiliza maoni ya wananchi juu ya mgogoro wa mipaka uliopo katika mtaa huo ambapo wananchi - hawaelewi kama wanahudumiwa na ipi kati ya Ubungo na Kisarawe ili kuondoa mikanganyiko iliyopo sasa.

Akiongea wakati wa mkutano huo, Mkuu wa Wilaya ya Ubungo Hashimu Abdallah Komba amewaeleza wananchi kuwa timu hiyo itajumuisha wataalamu na wananchi 8 kutoka pande zote mbili lengo ikiwa ni kujiridhisha na kupata uelewa wa pamoja kuhusu mipaka ya mtaa huo kwa mujibu wa tangazo la Serikali (GN) ya awali ya mwaka 1974 na marekebisho GN ya mwaka 2019 ili kuondoa utata uliopo sasa lakini pia wananchi kujua wanahudumia na mamlaka ya ut-

Inaendelea Ukurasa wa 23......................



Inaendelea ......................................

awala wa Wilaya ipi.

"Hii timu itafanya kazi kwa muda wa wiki tatu na baada ya hapo utaitishwa mkutano wa wananchi kwa ajili ya kupata mrejesho na kutoa maamuzi kuhusu mipaka ya eneo na hivyo tunaamini mgogoro huu tutakuwa tumeumaliza na wananchi mtaendelea kufurahia maisha kwa kufanya shughuli zenu za maendeleo kwa uhuru na Amani" alieleza Mhe. Komba.

Pamoja na kuunda timu hiyo maalumu, Mhe. Komba amewataka wananchi washikamane na kushirikiana kwani wao ni wamoja badala ya kutenganishwa na migogoro ya mipaka kwani inaweza kubadilishwa wakati wowote kulingana na ongezeko la watu, hivyo tusigombane kwa ushawishi wa watu wachache wenye maslahi yao binafsi.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe Mhe. Fatma Almasi Nyangasa aliwaeleza wananchi kuwa katika kipindi hiki cha Mtaa wa king'azi wenye mgogoro utahudumiwa na wenyeviti wawili wa King'azi na Kisopwa mpaka pale mgogoro utakapotatuliwa.

Aidha, Mhe. Nyangasa aliwaonya Wenyeviti hao kutojihusisha na uuzaji wa ardhi kwani hicho ndio chanzo kikubwa cha mgogoro huo uliopo sasa.




# TIMU YA MPIRA WA PETE UBUNGO YATOKA SARE DHIDI KINONDONI

Na Mwandishi wetu

Timu ya mpira wa Pete Manispaa ya Ubungo imetoka sare kwa goli 22 - 22 dhidi ya timu ya mpira huo ya Manispaa ya Kinondoni katika mechi iliyochezwa leo tarehe 04/10/2023 ndani ya viwanja vya Manispaa ya Kinondoni.

Akiongea baada ya kumalizika kwa mechi hiyo Mhe. Songoro Mnyonge Mstahiki Meya wa Manispaa ya Ubungo amezipongeza timu hizo mchuano huo ambao umepelekea kutoka sare na kuwataka kuongeza bidii ya mazoezi ili kuendelea kuwa imara.

“Ubungo na Kinondoni ni watoto wa baba mmoja na hilo limejidhihirisha kwenye hii mechi fanyeni mazoezi ya kutosha ili kupata ushindi kwenye mechi zote mtakazocheza” Alisema Songoro.

kwa upande wake Afisa Utamaduni wa Manispaa ya Ubungo Kasim Semfuko ameitaka timu ya Manispaa hiyo kucheza mechi nyingi zaidi ili kuweza kujiboresha sambamba na ufanyaji mazoezi ipaswavyo ili kuweza kushinda mashindano ya SHIMISEMITA 2023 yanayotarajiwa kuanza hivi karibuni.

Mnamo tarehe 18 Oktoba, 2023 Mashindano ya Shirikisho la Michezo Serikali za Mitaa Tanzania “SHIMISEMITA” yataanza rasmi Mkoani Dodoma ambapo timu mbalimbali za Michezo za Halmashauri kote Nchini zitapata fursa ya kushiriki mashindano yao.



## MECHI YA KIRAFIKI UBUNGO 1 VS TEMEKE 1

Na Mwandishi wetu

Mapema asubuhi ya Oktoba 07, 2023 timu ya mpira wa miguu ya Manispaa ya Ubungo imecheza mchezo wa kirafiki dhidi ya timu ya Manispaa ya Temeke katika uwanja wa Mwembeyanga

Mchezo huo uliokuwa wa kuvutia kwa pande zote mbili umemalizika kwa sare ya goli moja kwa moja

Timu ya Manispaa ya Ubungo itashiriki mashindano ya SHIMISEMITA yatakayofanyika kuanzia Oktoba 18, 2023 jijini Dodoma.

Mwenyekiti wa Klabu ya Michezo na kocha wa timu ya Manispaa ya Ubungo Mwalimu Boki Masoud amesema kuwa ameridhishwa na maandalizi ya kikosi chake na kikosi kipo tayari kwenda kupe-perusha vyema bendera ya Manispaa ya Ubungo katika mashindano hayo

Mpaka sasa Timu ya Manispaa ya Ubungo imecheza michezo ya kirafiki mitatu na haijapoteza mchezo wowote

Ubungo Fc 2 Vs 2 St. Anne
Ubungo Fc 2 Vs 1 Kinondoni Fc
Ubungo Fc 1 Vs 1 Temeke Fc



## BARAZA LA MADIWANI HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO






WATUMISHI MBALIMBALI WA MANISPAA YA UBUNGO



HALIUZWI

**OFISI YA MKURUGENZI WA MANISPAA**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO**

**S.L.P 55068**

**DAR ES SALAAM**

UBUNGO yetu

FAHARI YETU

**Jarida hili limehaririwa na kusanifiwa na;**
**Joina Nzali**
**Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini.**
**Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo.**
**Limeandaliwa na;**
**Martha Julius (Afisa Habari-UMC)**
**Twagile Sanga (Afisa Habari- UMC)**

Barua pepe; md@ubungomc.go.tz
Tufuatilie kupitia kurasa za Ubungo Manispaa/ Tovuti: www.ubungomc.go.tz